



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA  
WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI  
(RITA)



## TANGAZO KWA WAFUNGISHAJI NDOA

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) umefanya maboresho katika mifumo ya kutoa huduma zake kwa wananchi kwa lengo la kuongeza ufanisi na wigo wa upatikanaji wa huduma kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa **eRITA** unaomuwezesha mwananchi kutuma maombi ya huduma popote alipo. Huduma zinazopatikana kidigitali kuititia **eRITA** ni Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka pamoja na Bodi za Wadhamini.

Kabidhi Wasii Mkuu na Msajili Mkuu wa Ndoa na Talaka anatoa wito kwa wafungishaji ndoa wote kujisajili kuititia **eRITA** kabla ya tarehe **10/03/2024** ili kuweza kupata leseni ambazo zinatoka kwa mfumo wa kidijitali. Wito huu unawahu wafungishaji ndoa walio na leseni hai na leseni zilizokwisha muda wake ambazo zilitolewa kabla ya kuwepo kwa mfumo wa kutoa huduma za ndoa kidijitali.

Ili kujisajili, ingia katika tovuti ya Wakala **www.rita.go.tz** kisha bofya kitufe kilichoandikwa eRITA na baada ya kuingia katika mfumo bofya na kuchagua Huduma ya Ndoa na Talaka kisha fuata maelekezo utakayopewa ili kukamilisha maombi ya huduma unayohitaji.

**ZINGATIA:** Wafungishaji Ndoa walio na leseni hai hawatahitajika kulipia ada Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kuititia namba ya simu 0800 117 482

Imetolewa leo tarehe 10 Disemba, 2023

Irene J. Leslie  
NAIBU KABIDHI WASII MKUU